SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 16)

SHERIA NDOGO ZA (UDHIBITI WA UCHAFUZI WA MAZINGIRA) HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA 2014

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Halmashauri ya Jiji la Tanga za (Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira), 2014 na zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Jiji la Tanga mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hizi, maneno yafuatayo yatamaanisha:-

"Ada" Maana yake ni malipo yatakayolipwa kwa mujibu wa Jedwali la pili la Sheria ndogo hizi;

"Adha" Maana yake ni hali yoyote mbaya yenye kuleta madhara au kero juu ya Afya ya watu na Viumbe hai kwa ujumla;

"Afisa Muidhiniwa" Maana yake ni mtu yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hizi;

"Afya" Maana yake ni hali timilifu ya Kimwili, Kiakili, Kimazingira na Kijamii;

"Bafu" Maana yake ni chumba maalum kilichojengwa kwa madhumuni ya kuogea;

"Biashara" Maana yake ni aina yoyote ya shughuli za kiuchumi inayomwingizia kipato mtu;

"Chakula" Maana yake ni kitu chochote kinacholiwa na binadamu ikijumuisha maji na dawa;

"Choo bora" Maana yake ni Choo cha lindi chenye shimo lililojengwa madhubuti au choo chochote cha maji chenye Sakafu imara, Banda Imara la kudumu, kimeezekwa, kina mlango imara kama cha lindi kimeongezwa bomba la kutoa hewa chafu na chenye mfuniko kwenye tundu la choo;

“Chukizo la afya” Maana yake ni kitu chochote kinachoweza kuleta kinyaa machoni kwa kuona, kunusa, hewa chafu, madhara au kuhatarisha afya za jamii au binadamu’

“Halmashauri” Maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Tanga “

“Huduma” maana yake ni huduma ya kukusanya, kusafirisha na kutupa taka katika Dampo linalokubaliwa;

“Jengo” linalohusisha nyumba yoyote, Kibanda, Conteina, jengo lililochakaa, jengo lisilotumika, hema na jengo la aina yoyote ambayo haikutajwa;

“Jiji” Maana yake ni Jiji la Tanga

“Kaya” Maana yake ni familia moja inayoishi aidha kwenye nyumba nzima au ndani ya chumba/vyumba ndani ya Halmashauri;

“Kibali cha afya” Maana yake ni Kibali kinachotolewa na Halmashauri kuthibitisha uwepo wa usafi na usalama wa afya katika maeneo ya kibiashara na kwa watoa huduma mbalimbali katika Halmashauri;

“Kituo cha maji machafu” Maana yake ni sehemu maalum iliyotengenezwa kwa ajili ya ukaguzi wa Mfereji, Kituo hiki kitakuwa na mfumo usioruhusu hewa kutoka **(Airtight Cover);**

“Kituo cha taka” Maana yake ni Kizimba cha taka ambacho kimewekwa na Halmashauri kwa madhumuni ya jamii inayoishi au inayofanya biashara jirani kuweka taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi kwenye Dampo rasmi la taka ngumu la Halmashauri ya Jiji;

“Kiwanja” Maana yake ni ardhi yoyote, Kiwanja kilichopimwa au kisichopimwa;

“**Kizimba”** maana yake ni kituo cha kukusanyia au kuhifadhia taka kwa muda ili zisafirishwe kutupwa kwenye dampo la Jiji.

“Mabwawa ya maji taka” Maana yake ni Mabwawa yaliyojengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi maji taka yanayotokana na kuosha vyombo, kufua nguo, kuosha nywele n.k.

“Maji taka” Maana yake ni maji machafu;

“Mazalio ya Wadudu” Maana yake ni sehemu ambayo Wadudu hufanya Mazalia au kuishi kwa minajiri ya kufanya mzunguko wa maisha na baadae huleta maafa;

“Mifugo” Ina maana Ng’ombe, Punda, Nguruwe, Mbuzi, Kondoo, Kuku au Mnyama yeyote afugwaye;

"Mkurugenzi" Maana yake ni mtu yeyote anayeshikilia nafasi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga kwa wakati huo, na ni pamoja na mtumishi yeyote wa Halmashauri atakayekuwa ameteuliwa kufanya kazi kwa niaba yake chini ya Sheria Ndogo hizi;

"Mtaa" Maana yake ni Mtaa, barabara za aina zote, maeneo ya Umma na maeneo ya wazi;

"Mtandao wa maji taka" Maana yake ni mfumo wa bomba kuu lililjengwa kwa madhumuni ya kupokea na kusafirisha taka miminika toka kwenye Mifereji ya maji na kuyapeleka kwenye Mabwawa ya maji taka;

"Mtu" Neno hili litajumuisha Binadamu, Kampuni, Kikundi cha watu, Kikundi cha Kijami, Kikundi cha kibiashara, Shirika la Umma au la Serikali, Shirika lisilo la Kiserikali na kundi lolote la watu lenye malengo yanayofanana;

"Mzalishaji wa maji taka" Maana yake ni mtu yeyote ambaye shughuli zake kwa namna moja ile huzalisha maji taka;

"Mzalishaji wa taka ngumu" maana yake mtu yeyote ambaye katika kutekeleza shughuli zake huzalisha taka ngumu;

"Nyumba ya kuishi" Maana yake ni jengo lolote ambapo Kaya inaishi;

"Pipa la taka" Maana yake nji chombo chochote chenye mfuniko kinachoweza kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa Majumbani, Mitaani, sehemu za biashara, Maofisini ili zisisambae na kuchafua mazingira;

"Taka za biashara" Maana yake ni aina yeyote ya taka ambazo hupatikana au hutokana na shughuli mbalimbali za kibiashara;

"Taka za bustani" Maana yake ni taka zitokanazo na kufyeka majani, kukata miti au kupalilia bustani za nyumbani, mitaa au kwenye bustani za maeneo ya umma.

"Taka za hatari" Ni aina yeyote ya taka ambayo kwa njia fulani hubaki kwenye mazingira na hatima yake ni kusababisha madhara kwa afya ya jamii. Taka za aina hii hujumuisha taka zitokanazo na shughuli za Hospitali "X-ray films, vitu vya Mionzi hatari, vitu vyenye ncha kali kama vile Sindano, Chupa, Mecury, Madawa mbalimbali, Mabasi, Vyuma, Kemikali, Gesi mbalimbali n.k;

"Taka za majumbani" Zitajumuisha mabaki ya vyakula, maganda ya matunda, majivu, marupurupu ya nguo, karatasi za aina mbalimbali na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa;

"Taka miminika" Maana yake ni maji yaliyokwisha tumika au kuchafuliwa kwa namna yoyote ile. Maji hayo yanajumuisha maji machafu toka chooni,

bafuni, jikoni, viwandani, maji yaliyooshea vyombo, maji yaliyofuliwa nguo, kuosha nywele, kuoshea vyakula na yaliyopigiwa deki n.k;

"Taka nzito" Mana yake ni masalia ya Magari/Pikipiki/Baiskeli mabovu, Mashine za kufulia mbovu, Friji mbovu, Komputa mbovu, Runing mbovu, vifaa vya ujenzi ambavyo vimechakaa au kuharibika na vingine vya aina hiyo;

"Taka ngumu" Maana yake ni taka zisizomiminika zitokanazo na shughuli za Majumbani, Shambani, Bustani, Biashara, Viwanda na Hospilini;

"Taka za shambani" Maana yake ni taka za aina zote zitokanazo na kuvuna Mazao, ufugaji wa Wanyama, ufugaji wa Ndege na mizoga ya Wanyama au Ndege;

"Taka za Viwanda" Mana yake ni aina yoyote ya taka ambazo hutokana na uzalishaji wa shughuli mbalimbali za Viwandani;

"Uchunguzi wa Afya" Mana yake ni hali ya mtu kupima afya yake kwa kuchukuliwa vipimo vya ndani na nje ya mwili ili kubaini kuwepo kwa Vijidudu vya magonjwa vinavyoweza kuleta maambukizi;

"Ufugaji ndani" Mana yake ni ufugaji wa Mifugo ndani ya eneo lililoruhusiwa tu;

"Ushuru" Maana yake ni malipo yatakayo lipwa kwa mujibu wa jedwali la kwanza, tatu nan ne la Sheria Ndogo hizi;

"Wakala" Maana yake ni mtu yeyote ambaye ameteuliwa na Halmashauri kukusanya na kutupa taka katika Dampo linalokubaliwa kwa niaba ya Halmashauri kusimamia Sheria Ndogo hii au Kifungu chochote.

Mamlaka ya Halmashauri kukagua mazingira

3. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukagua nyumba yoyote, kiwanja, barabara, njia ua uchochoro wowote, mfereji wa maji ya mvua au ardhi katika eneo lolote la Halmashauri muda wowote na kuchukua hatua zozote itakazoona zinafaa katika kuweka mazingira kuwa kwenye hali ya usafi.

Wachuuzi na wafanya-biashara kutunza mazingira

4. Wachuuzi na Wafanyabiashara Mitaani, watatunza mazingira yanayozunguka maeneo yao ya kazi, ikiwa ni pamoja na jengo la biashara, kiwanja, mifereji ya maji na mazingira yanayozunguka eneo la kazi.

Kutupa taka katika eneo lililotengwa kwa ajili hiyo

5. (1) Ni marufuku kutupa taka au uchafu wowote au kuacha kuwepo taka au uchafu kwenye nyumba, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua barabara au eneo linalopakana na nyumba yoyote au ardhi yoyote au karibu na maeneo ya nyumba au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo;

(2) Kila Kaya iliyoko ndani ya Halmashauri itakuwa na Pipa maalum la ukubwa wa kutosha lenye Mfuniko litakalotumika kutupia taka ngumu;

(3) Ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kutupa taka za biashara, viwandani, majumbani, bustani na taka za shambani katika eneo lisilotengwa kwa shughuli hiyo;

(4) Taka ngumu zote zitakusanywa na kuhifadhiwa kwenye Pipa maalum lenye Mfuniko;

(5) Mapipa ya taka yakijaa, Wamiliki watamwaga taka zilizojaa kwenye Kizimba kilichoko katika au kwa kufuata utaratibu maalum uliokubaliwa na Halmashauri ya Jiji;

(6) Halmashauri ya Jiji itaweka utaratibu wa kusafirisha taka kutoka kwenye Vizimba na kutupa kwenye Dampo la Jiji kwa ratiba ambayo itafuatwa na jamii, mtu yeyote atakayekwenda kinyume na ratiba atakuwa ametenda kosa;

(7) Kila mwenye nyumba au Kaya atawajibika kusafisha mfereji wa maji ya mvua uliopita karibu na nyumba yake na kuhakikisha kuwa Mfereji na maeneo yanazozunguka nyumba yote yanakuwa safi wakati wote;

(8) Chombo chochote kilichobeba taka ngumu kinatakiwa kiwe kimefunikwa kiasi cha kuzuia taka ngumu zisionekane wala kumwagika chini na kuleta adha kwa watu na uchafuzi wa mazingira kwa ujumla;

(9) Bila kuathiri kifungu kingine chochote cha Sheria Ndogo hizi, Mmiliki wa chombo chochote kitakachosafirisha taka ngumu bila kufunikwa au kutofunikwa ipasavyo atalazimika kulipa kiasi cha shilingi 200,000/= ikiwa ni gharama ya kusafisha mazingira kutokana na uchafuzi wa taka ngumu zilizodondoka;

(10) Chombo chochote kitakachosafirisha taka ngumu bila kufunikwa au kutofunikwa ipasavyo kitakamatwa na Halmashauri na iwapo Mmiliki wake atashindwa kulipa gharama iliyotajwa katika Kifungu Kidogo cha (9) ndani ya siku kumi na nne kuanzia siku ya kukamatwa; Halmashauri itakiuza chombo hicho kwa njia ya mnada ili kufidia gharama hizo na kiasi chochote kitakachobaki kitarudishwa kwa Mmiliki.

Ada ya taka ngumu

6. (1) Kila Kaya, Taasisi zote wenye Viwanda na Wafanyabiashara za aina zote ndani ya Halmashauri watalipa ada kama ilivyoanishwa kwenye jedwali la kwanza na la tatu la Sheria Ndogo hizi ikiwa ni gharama ya kusafirisha taka ngumu kutoka kwenye nyumba hadi sehemu iliyotengwa maalum kwa ajili ya kutupa taka ngumu;

(2)Halmashauri inaweza kuteua Wakala wa kukusanya ada iliyotajwa katika Kifungu Kidogo cha (1);

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukusanywa ada ya taka ngumu bila Kibali cha maandishi cha Halmashauri;

(4) Muda wa mwisho wa kulipa ada ya taka ngumu ni tarehe tano ya mwezi unafuata mwezi unaolipwa ada. Baada ya hapo ada italipwa pamoja na adhabu ya 20% ya ada;

(5) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, taka nzito (Bulk Waste) zitasimamiwa kama taka nyingine, isipokuwa ada ya kusafirisha na kutupa kwenye Dampo la Jiji itaongezeka kulingana na Halmashauiri itakavyoona inafaa;

(6) Kila mwenye jengo la biashara au Mpangaji wa jengo la biashara ndani ya Soko atalipa nyongeza ya shilingi 200/= kila siku kwa ajili ya kusafirisha na kutupa taka katika Dampo la Jiji.

Kutiririsha maji taka

7. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutiririsha au kumwaga au kuruhusu au kusababisha kutitirishwa au kumwagwa maji taka barabarani, uchochoroni kwenye mifereji mtoni, vyanzo vya maji au sehemu yoyote isiyotengenezwa kuhifadhi maji taka;

(2) Kila Kiwanda kilichopo ndani ya Halmashauri kinachozalisha maji taka kinatakiwa kuunganisha maji taka kwenye mtandao wa maji taka au kujenga Mabwawa kwa ajili ya kutakasa au kuhifadhi maji taka ya kiwanda;

(3) Nyumba zote isipokuwa nyumba zinazotumika kama Kiwanda, zinatakiwa kuwa na Karo la kuhifadhia maji taka. Kila mwenye nyumba anawajibika kunyonya maji taka pale karo linapojaa na ni marufuku kwa mtu yeyote kuacha karo kujaa na kutiririsha maji taka barabarani au sehemu yoyote isiyoruhusiwa;

(4) Mtu yeyote atakayehitaji huduma ya Halmashauri ya kusafirisha na kumwaga maji taka kutoka kwenye karo la maji taka lolote atalipa ada ya huduma hiyo kama ilivyotolewa kwenye Sheria Ndogo hzi.

Matumizi ya vyoo bora safi

8. (1) Kila mwenye nyumba katika eneo la Halmashauri atakuwa na choo bora na safi kwa matumzi ya wakazi wa nyumba hiyo;

(2) Kila Mmiliki wa nyumba inayotumika kwa shughuli za Ibada, Biashara, Hoteli, Mgahawa, Nyumba ya kulala wageni, Baa, Klabu, Gereji au shughuli yoyote inayokusanya watu wengi kwa pamoja ataweka na kutunza vyoo vya kutosha kwa jinsia za Kiume na Kike;

(3) Kila mwenye nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa choo chake ni kisafi na kinafanyiwa usafi kila siku, kupulizwa dawa ya kuua wadudu mara kwa mara na kunyonywa uchafu/majitaka (empting) pale kinapojaa kama choo cha shimo;

(4) Iwapo katika ukaguzi utakaofanywa kwa mujibu wa Kifungu Kidogo cha (3) itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo au choo kilichopo hakifai kwa matumizi ya binadamu. Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuchukua hatua yeyote inayoona inafaa ikiwa ni pamoja na kuzuia nyumba hiyo isitumike hadi choo kitakapojengwa au kurekebishwa.

Kudhibiti mazalia ya wadudu

9. Kila mwenye nyumba anawajibika kuhakikisha kuwa hakuna mazalio ya wadudu kama vile Mbu, kwenye nyumba yake au karibu na nyumba yake kwa kuondoa maji yaliyokusanyika, kufyeka majani na kuharibu kitu chochote kinachoweza kuwa mazalio ya wadudu.

Kufanya biashara kwenye eneo lisiloruhusiwa

10. Ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya biashara ya aina yeyote ikiwa ni pamoja na biashara za kutembeza, kuuza vyakula kwenye maeneo ambayo hayakutengwa rasmi kwa shughuli za biashara ya aina hiyo.

Kibali cha Afya kutolewa kabla ya Leseni ya biashara

11. (1) Kila mwenye jengo au kiwanja kilichokusudiwa kutumika kwa biashara, ataomba Kibali cha afya cha Halmshauri kabla ya kuomba Leseni ya Biashara;

(2) Hakuna biashara yoyote itakayoendeshwa katika eneo la Halmashauri bila Kibali cha Afya halali cha Halmashauri;

(3) Kwa kila mwaka wa fedha, Halmashauri itaweka ada za Vibali vya afya ambazo vitatekelezwa kwa mtu yeyote atayetaka kuweka biashara ndani ya eneo la Halmashauri;

(4) Mtu yeyote atakayeshindwa kulipia kadi ya afya kwa muda unaotakiwa kama ilivyo kwenye jedwali la pili la Sheria hizi, atalipa nyongeza na faini ya 50% ya ada ya mwaka.

Kudhibiti ubora wa vyakula

12. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza vyakula kwenye eneo lolote la Halmshauri bila Kibali cha maandishi cha Halmashauri;

(2) Mtu yeyote anayetaka kufanya biashara ya kuuza chakula ataandika ya maombi, iwapo Halmashauri itaridhika na maombi yake atapatiwa kibali;

(3) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kufuta Kibali kilichotolewa kwa mujibu wa Kifungu Kidogo cha (2), iwapo aliyepewa Kibali atakiuka masharti ya Kibali chake.

Utunzaji wa miti

13. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata au kuharibu mti wa aina yoyote ndani ya Halmashauri bila Kibali cha Halmashauri;

(2) Bila kuathiri ujumla wa Kifungu cha (22) cha Sheria Ndogo hizi, mtu yeyote atakayekata au kuharibu mti wowote atawajibika kulipa gharama zitakazoainishwa na Halmashauri za kupanda na kukuza mti mwingine.

(3) Kila mwenye nyumba katika eneo la Halmashauri atapaswa kupanda na kutunza miti ya kivuli au matunda

isiyopungua mitatu katika eneo lake. Miti itakayopandwa isiwe na madhara kwa mazingira au miundombinu ya aina yoyote;

(4) Mtu yeyote mwenye bustani atatunza bustani yake kwa urefu wa maua usiozidi meta tano.

(5) Mtu yeyote atakayepalilia bustani au kukata miti, atawajibika kutupa taka za bustani ndani ya masaa ishirini na nne kuanzia alipopalilia bustani au alipopunguza urefu wa miti.

Kunya au kukojoa hovyo

14. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kunya au kukojoa katika eneo ambalo siyo choo;

(2) Halmashauri inaweza kumuamuru Mmiliki au Mwangalizi wa nyumba ya kuishi au jengo lolote kupakua na kutupa mavi na maji taka mahali paliporuhusiwa au bwawa lililoruhusiwa;

(3) Mtu yeyote atakayepakua na kutupa mavi na maji taka bila Kibali cha maandishi cha Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

Mmiliki au mwangilizi wa kiwanja au jengo lisilotumika kutekeleza sheria ndogo hizi

5. (1) Mmiliki au Mwangalizi wa Kiwanja ambacho hakitumiki au hakijaendelezwa au jengo lolote lisilotumika atatunza kiwanja au nyumba kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na Halmashauri itajiridhisha na utunzaji huo, endapo Halmashauri haitaridhika mtu au Mwangalizi anayehusika atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa kupimwa Afya wahudumu

16. (1) Wahudumu wote katika Hoteli, Migahawa, Baa za aina zote za Kigeni au Kienyeji, Bucha, sehemu za kuokea Mikate, nyumba za kulala wageni, Grosari au watu wote wanaoshughulika na vyakula vilivyotengenezwa kwa ajili ya kuuza; watapaswa kupimwa afya zao kila baada ya miezi sita na watalazimika kulipia ada ya upimaji wa afya;

(2) Kila Mmiliki wa Hoteli, Migahawa, Baa za aina zote za Kigeni au Kienyeji , Bucha, sehemu za kuokea Mikate, nyumba za kulala wageni, Grosari au eneo lolote linaloshughulika na vyakula vilivyotengenezwa kwa ajili ya kuuza atawajibika kuhakikisha kuwa Wahudumu wake wamepimwa afya zao kabla ya kuanza kazi na atahakikisha kuwa wanapimwa afya zao kila baada ya miezi sita;

(3) Bila kuathiri ujumla wa Kifungu cha (22) cha Sheria Ndogo hizi, Mmiliki yeyote atakayeruhusu Mhudumu yeyote kufanya kazi bila kupimwa afya yake atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini kwa kila siku ambayo Mhudumu huyo atafanya kazi bila kupimwa afya yake.

Kutunza vyanzo vya maji

17. (1) Hairuhusiwi kwa mtu yeyote kunawa, kuoga au kufulia nguo karibu au kwenye chanzo cha maji kama vile chemuchemu, kisima au chanzo kingine chochote cha maji au kunywesha Mifugo kwenye chanzo cha maji kama vile chemuchemu, kisima au chanzo kingine chochote cha maji au kunywesha au kuruhusu kunywesha mifugo kwenye chanzo cha maji kinachotumika kwa matumizi ya nyumbani ila kwenye sehemu iliyotengwa kwa shughuli hizo;

(2) Ni marufuku kujenga Boma la Mifugo karibu au kuruhusu mkojo au maji machafu kuelekea kwenye au karibu na chanzo cha maji kwa matumizi ya binadamu.

Udhibiti wa mifugo Mijini

18. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kufuga mfugo wa aina yoyote bila Kibali cha Halmashauri;

(2) Mtu yeyote atakayefuga Mfugo wa aina yoyote bila Kibali cha Halmashauri au kukiuka masharti ya Kibali chake, atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi Laki tatu;

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuacha Mifugo au kusababisha Mifugo kuachwa kuzurura ovyo Mitaani, Barabarani au kuchungwa kwenye eneo lolote lisiloruhusiwa;

(4) Mfugo wowote utakaokutwa ukizurura au kuchungwa kwenye eneo lisiloruhusiwa utakamatwa na Halmashauri na mwenye Mfugo atalazimika kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini kwa kila Mfugo uliokamatwa na gharamza za kukamata na kutunza Mfugo huo ndani ya muda utakaopangwa na Halmashauri;

(5) Mfugo wowote utakaoshindwa kukombolewa ndani ya muda wa siku saba, utauzwa na Halmashauri kwa njia ya mnada ili kulipia faini, gharama za ukamataji na utunzaji wa Mfugo na kiasi chochote kitakachobaki atarudishiwa mwenye Mfugo;

(6) Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kutoa maelekezo yoyote wakati wowote kuhusu ufugaji na mtu yeyote atakayekiuka maelekezo hayo atakuwa ametenda kosa.

Kuzuia uoshaji hovyo wa magari

19. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuosha gari kwenye eneo ambalo halijatengwa rasmi kwa kazi hiyo.

Utoaji wa taarifa za magonjwa ya mlipuko

20. Mtu yeyote katika eneo la Halmashauri atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi iwapo atashindwa, atapuuza au ataacha kutoa taarifa ya uwepo wa Magonjwa ya Mlipuko kama vile Kipundupindu.

Uwezo wa kufifilisha kosa

21. (1) Mkurugenzi au Afisa Muidhiniwa anaweza kumtoza faini isiyozidi shilingi elfu hamsini kwa kila kosa mtu yeyote aliyetenda kosa na kukiri kwa maandishi;

(2) Mtu aliyefanya kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, atakiri kosa hilo kwa kujaza fomu maalum zitakazotolewa na Halmashauri.

Uchimbaji na usafirishaji wa kokoto, mawe na mchanga

22. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba kokoto, mawe au mchanga katika eneo la Halmashauri bila Kibali cha maandishi cha Halmashauri;

(2) Mtu yeyote anayetaka kuchimba mchanga, kokoto au mawe katika eneo la Halmashauri atatuma maombi yake kwa njia ya maandishi na kulipia ushuru wa maombi haya kwa viwango vitakavyopangwa na Halmashauri;

(3) Halmasahuri itakuwa na Mamlaka ya kukataa maombi yoyote, iwapo itaona kuwa uchimbaji wa kokoto, mawe au mchanga utakuwa na athari za kimazingira;

(4) Mtu yeyote anayesafirisha mawe, mchanga au kokoto katika eneo la Halmashauri atahakikisha kuwa chombo anachotumia kusafirishia mchanga, mawe au kokoto kimefunikwa chote ili kuzuia mchanga, kokoto au mawe kumwagika na kuchafua mazingira;

(5) Chombo chochote kinachotumika kusafirisha mawe, mchanga au kokoto kwa kukiuka masharti ya Kifungu Kidogo cha (4) kitakamatwa na Halmashauri na Mmiliki wake atalipa shilingi 200,000/=, ikiwa ni gharama za uchafuzi wa mazingira kabla ya gari hiyo kuachiwa. Iwapo gharama hiyo haitalipwa ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kukamatwa chombo hicho; Halmashauri itauza chombo hicho kwa njia ya mnada kufidia gharama hizo na kiasi kitakachobaki atarudishiwa mwenye chombo.

Ushuru wa mawe, kokoto na mchanga

23. Kila mtu atakayesafirisha mchanga, kokoto au mawe katika eneo la Halmashauri atawajibika kulipa ushuru kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la nne la Sheria Ndogo hii.

Uteuzi wa Wakala

24. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua mtu au Wakala kusimamia Sheria Ndogo hizi.

Adhabu ya jumla

25. Mtu yeyote atakayekiuka Kifungu chochote cha Sheria Ndogo hii, atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia, kama hakuna adhabu maalum iliyoainishwa katika Kifungu kilichokiukwa, atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au Kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja Faini na Kifungo.

JEDWALI LA KWANZA
KIFUNGU CHA 6(1)

Viwango vya Ada ya Uzoaji na Utupaji Taka Ngumu

NA	*AINA YA JENGO*	*KIWANGO KATIKA SHILINGI KWA MWEZI*
1	Maduka ya jumla	15,000.00
2	Maduka ya rejareja	10,000.00
3	Taka za nyumbani	1,000.00
4	Viwanda vikubwa	100,000.00
5	Viwanda vya kati	50,000.00
6	Viwanda vidogo	30,000.00
7	Hoteli kubwa	100,000.00
8	Hoteli za kati	45,000.00
9	Nyumba za kulala wageni	25,000.00
10	Hospitali	50,000.00
11	Vituo vya Afya na Zahanati	30,000.00
12	Ofisi	30,000.00
13	Wakandarasi wa Majengo	50,000.00
14	Maduka ya Vifaa vya Magari	15,000.00
15	Ofisi za Mawakili	10,000.00
16	Ofisi za Wataalamu wa kuua Wadudu	10,000.00
17	Maghala makubwa	50,000.00
18	Maghala ya kati	30,000.00
19	Maghala madogo	20,000.00
20	Ofisi za Wahasibu/Wakaguzi na huduma za Kompyuta	20,000.00
21	Ofisi za Steshenari	10,000.00
22	Mgahawa	10,000.00
23	Taka za bustani	20,000.00
24	Biashara nyingine yoyote	10,000.00
25	Majumba ya Sinema	20,000.00
26	Mashine za Kusaga	20,000.00
27	Karakana	20,000.00
28	Mnada	20,000.00
29	Mashine za kushona	10,000.00
30	Usafirishaji	20,000.00
31	Vituo vya kuuza Mafuta ya Magari na Pikipiki (Filling Stations)	10,000.00
32	Mawakala	10,000.00
33	Ada ya kutupa taka kutoka kwenye Mkokoteni ndani ya Kizimba	5,000.00 kwa safari moja
34	Studio za Picha	10,000.00
35	Huduma za kufua na kunyoosha	10,000.00
36	Saluni ya Kiume na Kike	10,000.00
37	Duka la Dawa	15,000.00
38	Uwanja wa Maonyesho	10,000.00
39	Viwanja vya Michezo	20,000.00
40	Shule	20,000.00
41	Kituo cha Kutunza Watoto	20,000.00
42	Baa	40,000.00
43	Magenge	10,000.00
44	Mama Lishe	5,000.00
45	Stendi kubwa ya Basi	80,000.00
46	Stendi ndogo ya Basi	40,000.00
47	Ukarabati wa vifaa vya umeme	20,000.00
48	Vizimba vya Soko	200 kwa siku
49	Kutupa taka kwenye Dampo la Jiji	10,000.00 kwa trip

JEDWALI LA PILI
KIFUNGU CHA 11 (3)

Ada za Vibali vya Afya

NA	*AINA YA BIASHARA*	*ADA YA KADI YA AFYA (TSHS)*
1	Maduka ya rejareja	5,000.00
2	Maduka ya jumla	10,000.00
3	Migahawa	10,000.00
4	Zahanati	15,000.00
5	Maghala makubwa	20,000.00
6	Maghala ya kati	15,000.00
7	Maghala madogo	10,000.00
8	Hospitali	20,000.00
9	Stoo	4,500.00
10	Nyumba za kulala wageni	10,000.00
11	Ofisi	5,000.00
12	Bucha	5,000.00
13	Gereji	10,000.00
14	Famasi	15,000.00
15	Saluni za Kiume na Kike	5,000.00
16	Baa	10,000.00
17	Glosari zenye Pombe	10,000.00
18	Glosari zisizo na Pombe	5,000.00
19	Majumba ya Sinema	20,000.00
20	Majumba ya Video	10,000.00
21	Sonara	5,000.00
22	Huduma za Kufua na Kunyoosha	5,000.00
23	Mawakala	5,000.00

NA	*AINA YA JENGO*	*KIWANGO CHA SHILINGI KWA MWEZI*
24	Senta za Kurekodi	5,000.00
25	Huduma za kuchaji Beteri	5,000.00
26	Studio za Picha	5,000.00
27	Vituo vya kujaza Mafuta	15,000.00
28	Maduka ya vifaa vya Umeme na Vifaa vya Magari	5,000.00
29	Wakandarasi wa Ujenzi	15,000.00
30	Seremala	10,000.00
31	Mashine za Kusaga	5,000.00
32	Watoa huduma za Shajala	20,000.00
33	Viwanda Vikubwa	25,000.00
34	Viwanda vya Kati	15,000.00
35	Viwanda Vidogo	10,000.00
36	Hoteli ndogo	5,000.00
37	Uhasibu na huduma za Kompyuta	5,000.00
38	Ushonaji	20,000.00
39	Karakana	10,000.00
40	Uuzaji wa Mbao	10,000.00
41	Masoko ya Minada	5,000.00
42	Mashine za Kusindika	10,000.00
43	Wachuuzi wa Samaki	5,000.00

JEDWALI LA TATU
KIFUNGU CHA 3

Ada ya kupakua makaro kwa Kata zilizopo katikati ya Jiji ni TSHS. 30,000.00 na kwa Kata za pembezoni mwa Jiji ni Tshs. 40,000.00

JEDWALI LA NNE
(KIFUNGU CHA 23)

UJAZO WA GARI	*KIWANGO CHA SHILINGI*
TANI 0 – 7	2,000.00
TANI 7 – 10	5,000.00
TANI 10 NA KUENDELEA	7,000.00

Nembo na Mhuri wa Halmashauri ya Jiji la Tanga umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 12.ya mwezi 05 Mwaka 2014 na kushuhudiwa na:

JULIANA MALANGE

Mkurugenzi Halmashauri ya jiji la Tanga

OMARI GULEDI
Mstahiki Meya Halmashauri ya jiji la Tanga

Nakubali:
…….
Dodoma
Tarehe …….20……

Mh. Mizengo P. Pinda
Waziri Mkuu